



## **AZIMIO NA. 4/2018**

# **AZIMIO LA KURIDHIA MKATABA WA KUZUIA UENDELEZAJI, UZALISHAJI, ULIMBIKIZAJI WA SILAHA ZA KIBAIOLOJIA NA SUMU PAMOJA NA UANGAMIZAJI WAKE [THE CONVENTION ON PROHIBITION OF DEVELOPMENT, PRODUCTION AND STOCKPILING OF BACTERIOLOGICAL (BIOLOGICAL) AND TOXIN WEAPONS AND ON THEIR DESTRUCTION] WA MWAKA 1972**

---

**KWA KUWA**, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni Nchi Mwanachama wa Umoja wa Mataifa;

**KWA KUWA**, Nchi Wanachama katika Mkutano wake uliofanyika tarehe 10 Aprili, 1972 zilizimbia kuwa na Mkataba wa Kuzuia Uendelezaji, Uzalishaji, Ulimbikizaji wa Silaha za Kibaiolojia na Sumu pamoja na Uangamizaji wake;

**KWA KUWA**, Mkataba huu ulianza kutumika rasmi tarehe 26 Machi, 1975, na hadi kufikia Septemba, 2018 nchi 181 ambazo ni asilimia 97 kati ya nchi 187 zilizosainiwa mkataba huo zilikuwa zimeuridhia;

**KWA KUWA**, kwa muda mrefu kumekuwepo na madhara makubwa yanayosababishwa na matumzi ya silaha za Kibaiolojia na Sumu yakiwemo mauaji ya makusudi ya raia wengi, magonjwa kwa viumbe hai, uharibifu wa mazingira na athari nyingine kwa jamii na uchumi kwa ujumla;

**KWA KUWA**, nchi watu binafsi na taasisi mbalimbali zimekuwa zikiendelea kutengeneza, kumiliki na kutumia silaha hizi za Kibaiolojia na Sumu na kuendelea kusababisha madhara na kuiweka Dunia katika hali tete kiusalama;

**KWA KUWA**, kutokana na hali hii tete kiusalama, nchi wanachama wa Umoja wa Mataifa zilionna kuna umuhimu wa kuungana ili kwa pamoja kuchukua hatua za kuzuia uendelezaji, uzalishaji, ulimbikizaji wa silaha za Kibaiolojia na Sumu pamoja na uangamizaji wake;

**KWA KUWA**, katika kufikia azma hiyo nchi wanachama zilianza kusaini Mkataba wa Kuzuia Uendelezaji, Uzalishaji, Ulimbikizaji wa Silaha za Kibaiolojia na Sumu pamoja na Uangamizaji wake, ambapo Tanzania ilisaini mnamo tarehe 16 Agosti, 1972;

**KWA KUWA**, Mkataba huu wa kimataifa ambao umekuwa ukitekelezwa na nchi mbalimbali unahitaji kuridhiwa na Bunge ili uweze kutekelezwa na nchi yetu kikamilifu;

**KWA KUWA**, kwa kushirikiana na nchi nyingine katika kuzuia uendelezaji, uzalishaji, ulimbikizaji wa silaha za Kibailojia na Sumu pamoja na uangamizaji wake, nchi yetu itanufaika kama ifuatavyo:

- (a) kupata fursa ya kubadilishana taarifa za madhara yanayosababishwa na matumizi ya silaha hizi zikiwemo taarifa za magonjwa mbalimbali;
- (b) kupata uwezo wa kubaini mapema matukio yanayotokana na matumizi ya silaha za Kibailoji na sumu na viambato (*precursors*) vyake;

- (c) fursa ya kupata mafunzo na mialiko ya kitaalam kwa ajili ya kujenga uwezo wa kukabiliana na majanga yanayosababishwa na silaha hizo;
- (d) fursa ya kupata teknolojia mpya kupitia sayansi ya vimelea na bidhaa za Kibaiolojia na tafiti za wanyama, mimea na mazingira;
- (e) kupata uwezo zaidi wa kudhibiti na kusimamia ubora wa maabara za uchunguzi wa bidhaa mbalimbali za kibaiolojia;
- (f) kuweza kupiga hatua katika kutekeleza kanuni za afya za Umoja wa Mataifa za Mwaka 2005 zinazoweka masharti ya kuzitaka Nchi Wanachama kukinga matukio na magonjwa yote yanayoathiri afya za wananchi wake.

**NA KWA KUWA,** kwa kuridhia mkataba huu nchi yetu itatakiwa kutoa michango ya wanachama ambayo ni kiasi cha Dola za Marekani 100 kwa mwaka ambacho ni kiasi kidogo ikilinganishwa na manufaa yatakayopatikana;

**KWA HIYO BASI,** kwa kuzingatia manufaa yatokanayo na Mkataba huu na pia umuhimu wake kwa usalama wa taifa, Bunge hili katika Mkutano wa 13 na kwa mujibu wa Ibara ya 63(3)(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano ya Mwaka 1977 linaazimia kuridhia Mkataba wa Kuzuia Uendelezaji, Uzalishaji, Ulimbikizaji wa Silaha za Kibailojia na Sumu pamoja na

uangamizaji wake uitwao *"The Convention on Prohibition of Development, Production and Stockpiling of Bacteriological (Biological) and Toxin Weapons and on their Destruction"*.

**Limepitishwa na Bunge leo tarehe 15 Novemba, 2018**

Stephen Kagaigai  
**KATIBU WA BUNGE**